

JE! UNASADIKI HAYO?

 Na kabla hatujaomba, ningetaka kusema hili, ya kwamba jana jioni, naamini ndivyo, nilimwambia mama fulani, “Kama utafanya tu jinsi tumeagizwa kufanya, kwamba ingeninii...yule mtoto mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji, kingesinyaa.” Nacho kichwa cha mtoto kikasinjaa, jana usiku, nusu inchi kwa kipimo cha uzi. Kwa hiyo mama huyo akamleta hapa sasa.

² Sasa, sababu ya mimi kufanya hivyo, dada, ni kwa kusudi fulani. Unaona? Kama unaweza kuona kitu dhahiri kikitukia, hicho kitaifanya imani yako iongezeke uendelee kuamini. Wakati mwingine mimi hufanya hivyo kuninii tu, labda, kama vile kumwomba mtu asimame, apige hatua moja ama mbili, uisogeze mkono wako, chezesha kidole chako, kitu tu wanachoweza kufanya vinginevyo, kuwafanya tu waone kwamba yote ni sawa kabisa. Wanashikwa tu na wasiwasi na kuwazia halitatukia, bali linatukia wakati wote. Mnaona? Halina budi kutukia.

³ Ni wangapi wanaotaka kukumbukwa katika maombi, sasa? Mwaweza tu kuinua mikono yenu na kusema, “Bwana, tujalie”? Na tuinamishe vichwa vyetu.

⁴ Bwana, tunapousikia wimbo huu mzuri sana wa kale wa kanisa, ulioandikwa na rafiki yangu wa thamani, Paul Rader, “Amini Tu,” tunawazia sasa juu ya mvulana, aliyeletwa na baba zake kwa wanafunzi, si zaidi ya siku kumi baada ya Yesu kuwapa mamlaka ya kuwatoa pepo na kuwaponya wagonjwa, nao hawa hapa wameshindwa kabisa na ugonjwa wa kifafa. Ndipo wakamwona Bwana wetu akija. Basi yule baba akakimbia na kusema, “Bwana, uturehemu. Mwanangu amepagawa sana na pepo. Nilimleta kwa wanafunzi Wako wala wasingeweza kumponya.”

⁵ Yesu akasema, “Ninaweza, kama ukiamini. Amini tu.” Ee Mungu, hujabadilika hata kidogo tangu wakati huo: Wewe ni Mungu yeye yule mwenye upendo, mzuri, na mwenye huruma. Kama ulivyokuwa wakati huo, ndivyo ulivyo leo hii. Basi Bwana, kama huyo baba, sote tunalia, “Bwana, usaidie kutokuamini kwetu.” Ni rahisi sana; tunajikwaa tu juu yake, Baba.

⁶ Tunataka kukutolea shukrani na sifa kwa ajili ya kumgusa mtoto huyo mchanga jana usiku, kuona ya kwamba fuvu hilo la kichwa, ambalo limevimba, hiyo ni kusema, kwamba mfupa umejitokeza, lilipungua nusu inchi jana usiku. Tunashukuru kwa ajili ya hilo, Baba. Wakati tukijua ya kwamba madaktari wetu hawana chochote katika utafiti kwake, hakuna kitu wanachoweza kumfanyia; bali Wewe ungali ni Mungu, Bwana

wa hali zote. Tunakushukuru, Baba. Tunakushukuru kwa ajili ya uaminifu wa mama huyu, na utamu, na utii wa kuurudisha ule uzi na kuubandika kwenye kipande hiki cha karatasi, hapa, kuuonyesha umma ushuhuda wake kwa utukufu wa Mungu. Jalia mtoto wake aishi na awe mtoto wa kawaida, kwa utukufu Wako.

⁷ Angalia mikono hiyo yote iliyoinuliwa, Baba. Kila mmoja wao alikuwa na haja. Wangu umeinuliwa, pia, Baba, nina haja. Na kuna wengi hapa, katika mfano wa barua ama kwenye kasha hili, walio wahitaji, watu ambao kweli ni wahitaji. Na itimie, Bwana, kwamba kila mmoja atapokea ombi lao usiku wa leo. Jalia wauchukue ushuhuda wa mama huyu na kama mfano tu wa kuonyesha kwamba Wewe unaposema lolote, limekwisha. Ni . . . Wewe . . . Yote yatupasayo kufanya ni kulipokea na kulitekeleza. Ni kazi iliyomalizika.

⁸ Jalia, Bwana, kwamba kila moja ya barua hizi na lesio hizi, watu watakaowekewa hizi, na waponywe. Kila mmoja aliyeuinua mkono wake, Baba, na wapokee haja yao ya moyoni. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina. Mwaweza kuketi.

⁹ Nilitaka tu kuwaonyesha ule uzi hapa, ambao yule mama . . . Haya basi. A-ha. Kwamba kichwa cha mtoto huyo mchanga kilisinyaa kama Bwana alivyotuahidi kupitia Roho Mtakatifu jana usiku. Si Yeye ni wa ajabu? Kwa hiyo, inatupa ujasiri mwingi kuwa na imani na kuamini.

¹⁰ Sasa, wakati Yesu alipouambia ule mti, katika Marko 11:23, "Mtu asile kutoka kwako tangu sasa," huenda hakupaza sauti. Wakati ambapo, hakika, aliliendea kwa urahisi sana, mpaka wanafunzi Wake wakaninii tu . . . Nafikiri mmoja wao alimsikia. Ndipo ikaninii . . . Wakati yule mwenye kifafa, wakati alikuja mbele za Bwana Yesu, mvulana huyo alishikwa na kifafa kibaya sana kilichopata kumshika; labda, akaanguka chini kana kwamba amekufa, bali alitambua ya kwamba alikutana na Mtu ambaye alikuwa na imani kubwa mno kuliko wale mitume.

¹¹ Sasa, ningetaka mtu ambaye hakuamini katika uponyaji wa Kiungu aangalie jambo hili. Yesu alikuwa amewapa mamlaka ya kuwatoa pepo, nao walikuwa wameshindwa. Si kwamba hayo mamlaka yalikuwa yameshindwa, bali wao walikuwa wameshindwa. Yesu akawaambia:

"Kwa nini hatokuweza kumtoa?"

Akasema, "kwa sababu ya kutokuamini kwenu."

¹² Kanisa lingali lina mamlaka. Mungu kamwe hajawahi kuyaondoa mamlaka Yake kanisani, bali kanisa halina imani ya kutosha kuyatekeleza. Hivyo tu. Ni rahisi tu hivyo. Tunajaribu kulifanya gumu sana wakati mwingine, lakini kadiri unavyoifanya Injili rahisi, ndivyo utakavyokuwa na uhalisi zaidi, wakati unapoiendea kirahisi sana: Mungu alisema hivyo; hilo latosha; na hamna lingine. Na uamini tu, endelea.

¹³ Wakati Yesu aliposema, “Mtu asile kwako,” mbona, hayo majani yalikuwa ni mazuri na maangavu kama yalivyopata kuwa. Gome lilionekana vile vile, lakini kule chini kabisa ardhini kwenye hiyo mizizi, uhai ulianza kufifia.

¹⁴ Ndivyo ilivyo juu ya kansa, juu ya namna yoyote ya ugonjwa amba—ambao huenda unataka kuwazia. Unapoweza kulikubali Neno la Mungu, kule chini kabisa mizizini, huenda kansa ingaliko; mkono wako huenda ukawa mgumu vile vile. Hilo halina uhusiano wowote na uponyaji wa Kiungu. Ni, “Kama unaweza kuamini.” Unaona? Huko chini kabisa mahali fulani, tayari inafanya kazi.

¹⁵ Yesu alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Hilo si ni la kupendeza? Hilo lingetoka kwa Nani? Mwana wa Mungu, ambaye Maneno Yake... Mbingu na nchi zitapita, bali sasa—bali Maneno Yake hayatapita.

¹⁶ Sasa, njia pekee unayoweza kufanya hivyo, huna budi kuwa na lengo zuri na nia nzuri. Sasa, kama ningalitoka niende hapa nje na kusema, “Nitawaonyesha ninaweza kuuhamisha mlima huu, ‘Ng’oka, ewe mlima.” Kamwe haungeng’oka. La hashu. Haidhuru nilikuwa na kitu gani. Inabidi iwe... Kwanza huna budi kutafuta kujua mapenzi ya Mungu.

¹⁷ Hiyo ndiyo sababu, kwa kawaida katika mistari ya maombi, ni—ninawapata walio wagumu sana, ni kwa sababu ni kitu ambacho kimepitia kwenye mistari na kadhalika, na hapo ndipo linakurudia. Lakini mnaona, kama una dhambi isiyotubiwa... Ulipata kuona kisa, kabla sijamwagiza pepo mchafu kuondoka? Ninaangalia kisa hicho kwa makini sana nipate kuhakikisha hakuna kitu katika maisha hayo ambacho kingezuia chochote, mnaona, kwa maana kumbukeni, kwenye karama hizi, ungeweza kupata shida nazo.

¹⁸ Mungu, mnakumbuka wakati mmoja, alimpa nabii... alimfanya mtu fulani nabii, Musa, akamwambia ashuke aende, akaseme na mwamba. Naye nabii akashikwa na msisimko sana, akatoka akaenda, na akaupiga ule mwamba, ikinena juu ya udhaifu wa Kristo, kwamba ingempasa kufa mara ya pili ama kupigwa mara ya pili. Alikuwa na mamlaka ya kuyaleta, bali hayakuwa ni mapenzi ya Mungu.

¹⁹ Kamwe nisingeamini kwamba ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Eliya kwenda huko, maana hao watoto walikuwa wakimdhikiki kuhusu kuwa kipara, sidhani ilimpasa kufanya hivyo. Lakini alikuwa ni nabii, naye alikuwa na hasira, ndipo akaweka laana juu ya watoto hao na dubu wawili wa kike wakawaua watoto arobaini na wawili wasio na hatia. Mnaona? Lakini siamini alipaswa kufanya hivyo. Nalo lilininii tu—ninii tu... sisi... .

²⁰ Mungu, ninaamini leo hii, kabla hajaliweka kanisa Lake mamlakani, Yeye hulijaribu kanisa Lake aone yale litakayofanya.

²¹ Sisi...wakati mwingine, labda, Bwana akipenda nitakaporudi, tutakuwa na wakati wa kukiendea kindani kitu kama hicho, juu ya kitu kilicho karibu kutukia, ndipo tutajua mengi kukihusu basi.

²² Lakini endapo utasema tu neno, useme, “Bwana, ninaamini,” usitilie shaka, ulimaanishe moyoni mwako. . .

²³ Sasa, tuseme kwa mfano, nilikuwa kwenye bonde, na sininii...ninahubiria mamilioni ya watu, bali upande wa pili tu wa mlima pale, kuna kundi la watu mia moja, nao wanakufa pasipo kumjua Kristo. Vema, nina milioni moja hapa wa kuhubiria, lakini hata hivyo, kitu Fulani moyoni mwangu kinaniambia, “Vuka ukawaendee wale watu. Waendee. Wanaangamia.” Sitaki kwenda mimi, hata hivyo kuna kitu Fulani ndani yangu. Mnaona, huyo ni Mungu basi, akitenda kazi. Angalia lengo lake ni nini, angalia nia ya kwenda ni nini, sio kwa ubinafsi. . . Sasa, kama nikisema, “Vema. . .” Kama lengo langu la kwenda kule ni zuri, lakini basi nifike hapa na huu hapa mlima mkubwa, niseme, “Unajua, kama nikiupanda mlima huu na kuwaokoa hao watu wote mia moja, siku moja watafanya sanamu pale: Ndugu Branham, yule mmishenari mashuhuri.” Sasa, nia yangu si nzuri. Huo mlima hautaanguka. La, bwana.

²⁴ Lakini wakati nia yangu na lengo langu ni sahihi, na Mungu moyoni mwangu ananiongoza, nami siwezi kupanda mlima huo, kuzunguka mlima huo, kupitia chini ya mlima huo, ningesema, “Ewe mlima, ng’oka.” Labda utaninii. . . Ninaposema hivyo, na mara nikisema kwa roho mzuri kama huyo, nikiongozwa na Roho Mtakatifu, katika mapenzi ya Mungu, huenda kusianguke zaidi ya kijiko kimoja cha mlima huo, bali umeanza kuanguka. Kesho yake huenda kukaanguka ratili mbili. Kesho yake robo tani. Na labda katika mwezi mmoja, tani tano zianguke. Vipi basi? Huenda hata usiuone bado, bali unasogea, umeanza kuanguka. Nitakaa papo hapo na kuangalia jambo hilo likitukia, kwa maana Mungu alisema hivyo na hilo latosha tu.

²⁵ Unaweza kuwazia hilo juu ya mama yako pale usiku wa leo? Vema, kama utaliwazia, atapata afya. Vema. Hiyo ni kama tu utaamini: nena tu neno na udumu nalo. Unaona? Amini tu; lishikilie. Ni Uzima wa Milele.

²⁶ Sasa, kesho alasiri...Nilimwambia Billy, usiku wa leo, aachane tu na kadi za maombi, nami nilitaka kuzungumza. Ninakiri katika kweli, nimekuwa safarini tangu Januari, nchi za ng’ambo, na kurudi, huko Phoenix, moja kwa moja nyumbani, na kurudi, na yote kabisa. . . Huo utambuzi. . . Mpaka nimechoka sana ni vigumu kujua ninaposimama wakati mwingine. Karibu uniangamize.

²⁷ Halafu basi, sina budi kuondoka, na wao...ninyi—ninyi ndugu mlinialika nikae huku kwa siku zingine. Jinsi ninavyoshukuru kwa hilo. Hakika ninafikiri hili ni kundi zuri sana la wahudumu hapa. Laiti tungalikuwa na wakati mwingi zaidi wa ushirika. Bwana akipenda, nitarudi wakati mwingine. Hakuna lingine, ni kutoka tu kwenye kanisa moja hadi lingine na kupitia mjini na kuwatembelea ninyi nyote. Ningefurahi kufanya hivyo: lolote ningaliweza kufanya kuusaidia Ufalme wa Mungu, hiyo ni kusema, kama mnetaka nifanye hivyo. Na kurudi wakati mwingine na kuungana nasi na kufanya mkutano mzuri, wa kupendeza mahali fulani.

²⁸ Pia kumbukeni, ndugu zangu, nitakuwa nikiwaombea. Hilo ni jambo moja la hakika. Nami ninawatakeni nyote mniombee, ninyi nyote.

²⁹ Na sasa ni—nina... kesho asubuhi ni ibada za kanisa katika makanisa haya yote mazuri mbalimbali kote mjini.

³⁰ Sasa, baadhi ya makundi kutoka Jeffersonville yapo hapa. Baadhi ya marafiki wangu, mmoja wa wadhamini wangu wa kanisa, yupo hapa, Ndugu Fred Sothmann. Kamwe sijaweza kumwona mkutanoni. Na ndugu...Loo, wengine wengi wa marafiki wangu kutoka huko Jeffersonville, nani wangu... katibu wangu pale na—na wote wapo hapa, mahali fulani mkutanoni. Sijawaona bado.

³¹ Nanyi ndugu, kuna makanisa mazuri sana hapa jijini. Nanyi wageni wengine wote, tafuteni moja la hayo na mwende kwenye makanisa haya kesho. Yatawasaidia, nina hakika. Hao ni ndugu wanaoamini katika huduma ya namna hii. Hiyo ndiyo sababu wako hapa wameketi jukwaani na huku chini mahali hapa, kwa kuwa wanaiamini. Nami ninawathamini watu hao.

³² Bwana, bariki tawi hili la Wafanyabiashara wa Full Gospel hapa ambao—ambao waliudhamini mkutano huu. Kuna... Ninaamini hiyo ilikuwa ni kweli, waliudhamini mkutano huu. Ni—ninaenda mahali pengi wanapodhamini, kwa maana mle... Haitupasi kuwa jinsi hii, bali mara nyingi, ndugu huachilia tofauti ndogo ndogo: kama vile mtu kuamini kitu *fulani* kidogo; mwingine kitu *fulani* kidogo; kidogo inasababisha msuguanu ndogo na vidonda vya kale sana; vinapaswa kuwa vimepona wakati huu, bali kina—kina... Na kama ukininii... kama nikiwapata Wafanyabiashara wa Full Gospel, basi kwa namna fulani hilo husaidia kukifunga, nasi tunakusanyika, na tunakuwa na ushirika halisi pamoja, wakati mzuri kwelikweli. Nasi tunathamini hilo. Mungu na alibariki tawi hilo. Ninaamini Mungu aliliinua kwa kusudi fulani.

³³ Sasa...ndipo nilikuwa na majaliwa mazuri ya kuona makao ya Ndugu Oral Roberts hivi majuzi. Na jamani, mahali pakubwa mno, kitu cha kupendeza kweli. Ni—ni kumbukumbu la Pentekoste.

34 Kisha nikaenda huko kwenye makao ya Ndugu Tommy Osborn, mahali pengine pazuri sana, mtu mzuri sana wa Mungu, ambaye. . . Mimi na Ndugu Tommy tuko karibu, na Ndugu Oral, pia, ndugu wa karibu kweli, na tunapendana, na tunajaribu tuwezavyo kufanya kila tuwezacho kwa manufaa ya watu katika Ufalme wa Mungu.

35 Kwa hiyo hakika ninathamini hao watu wakiwa hapa katika jiji hili miongoni mwa watu hawa wengine wazuri mlio nao hapa. Ninyi kondoo mna wachungaji wazuri sana. Ninaninii tu, nitalisema namna hiyo. Bwana na aendeleo kuwa nanyi nyote ndilo ombi langu. Na sasa kesho alasiri, mimi. . . Ibada huanza saa ngapi, enyi ndugu? Saa nane u nusu. Hebu tuseme saa saba—saba au saba u nusu mnapaswa kuwa hapa kusudi wasizikatie ibada hizo zingine.

36 Sasa, kama hao wavulana hawajawaambia tayari, usiku wa leo wana vitabu, picha na kadhalika, na kanda, na santuri, na. . . za mikutano, nao wanaziua. Lakini hatutawaruhusu kuziua kwenye Sabato, kesho. Hamna vitabu wala chochote kitakachouzwa kesho. Kwa hiyo hatutaninii. . . kamwe hatukuruhusu hilo. Ingawa wengi walisema, “Umekosea vibaya sana. . .”

37 Naye mzee Baba Bosworth alizoea kuniambia, “Loo, Ndugu Branham, hapo umekosea,” bali hivyo ndivyo nionavyo mimi (Mnaona?), na na—najisikia. Kama ukitaka kimoja, watakupa kimoja, bali kama ukininii. . . Ila hatuwezi kuuza kwe—kwenye Sabato. La. Hivyo tu. Kama ninaamini hivyo, inanibidi kuliishi, ninii tu. . . Sina budi kuishi kwa nafsi yangu. Mnaona? Nami si—sina budi kuishi kwa imani yangu na kwa hiyo. . . Ama mnaweza kuagizia nyumbani, na, hata nyumbani, mpaka mahali hapo na kukipata.

38 Sasa usiku wa leo, loo, hebu sisi sote tusahau tu jambo hilo, loo, kwamba kuna kazi yoyote ya kufanywa, au chochote kile, ama masumbuko ya siku. Hebu na tuweke kando kila kitu, na kuangalia kwenye Neno kwa dakika chache, tuone kile Mungu angetunenea kupitia Neno Lake. Na hebu niombe kwamba Mungu atatupa tu baraka kubwa mno usiku wa leo.

39 Gene, waweza kunikamatia huyo? Waweza kunikamatia msichana huyo mdogo? Si yeye ni kitoto kirembo sana? Ungetaka kwenda nyumbani pamoja nami ukacheze na mtoto wangu Sara, mwenye kimo hiki? Loo, ungetaka? Ni—ningetaka ufanye hivyo. Yeye ni wa karibu tu kimo chako, naye ni kisichana cha Baba. A-ha. Hum. Nami najua u—unampenda Baba yako pia, sivyo? Mama? Loo, hakika unawapenda. Msichana mdogo aliye mrembo sana, nimeketi hapa, nikimwangalia. Macho madogo yanaonekana kama mashimo mawili yaliyochomelewa kwenye blanketi na—na maskini nywele za hudhurungi.

40 Ninawapenda sana watoto wadogo. Nina wasichana wawili wadogo nyumbani. Mmoja wao ni Rebeka na huyo mwingine ni Sara.

41 Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa nimeondoka. Wote ni wasichana wadogo wa Baba, mwajua, nami ninawapenda. Na mara wanapoingia sina budi kuwatupa mgongoni, na...ila tu Becky ameanza kuwa mkubwa mno kwa jambo hilo; ni mkubwa kama nilivyo mimi. Angeuvunja mgongo wangu sasa; yeye... bali angali ni msichana mdogo wa Baba, haidhuru. Na sasa, yapata mwaka mmoja zaidi, tunataka kumpeleka kwenye chuo cha Biblia mahali fulani na mbali na shule ya serikali.

42 Na basi, walikuwa wakimngojea Baba, mwajua, arudi nyumbani. Nilikuwa nje mkutanoni. Na kesho usiku watakuwa wakingojea hadi usiku wa manane ili nijaribu kufika kule. Na kwa hiyo, niliingia asubuni na mapema sana, yapata saa tisa ama kumi. Basi mama akaja mlangoni na kunikaribisha, nami nilikuwa nimechoka sana na kudhoofika, nikaninii...Hapa jukwaani, mimi...wakati ninii...ukiwa na upako unajisikia vizuri, bali mara huo unapokuondokea, hapo ndipo unapata shida. Ni wangapi walipata kujua hilo? Mbona, hakika ndivyo.

43 Angalieni. Eliya alipanda mlimani na kuagiza moto kutoka mbinguni, akaagiza mvua kutoka mbinguni, ndipo basi wakati Roho alipomwacha, alitangatanga nyikani siku arobaini ndipo Mungu akampata, amejificha pangoni mahali fulani.

44 Yona, alishuka akakaa akiwa hai katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, akatemwa ufukoni kisha akaenda kote akihubiri. Jiji zima likatubu na kumjia Mungu. Ndipo upako ulipomwacha, alipanda mlimani na kumwomba Mungu ayachukue maisha yake. Mnaona?

45 Nilisimama karibu na kaburi la William Cowper, si muda mrefu uliopita, aliyeandika ule wimbo maarufu tunaoutumia kwenye ibada yetu ya ushirika:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye vena za Imanueli.
Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa
chini ya gharika hilo...

46 Je! ulipata kusikia kile yeye...kilichompata? Baada ya huo uvuvio kumwondokea, alijaribu kupata mto akajiue.

47 Ninaishi moja kwa moja ng'ambo ya Makazi ya kale ya Kentucky. Naye Stephen Foster aliipa Marekani nyimbo zake za jadi zinazojulikana kuliko zote. Na wakati angeandika, uvuvio unamwingia, uvuvio huo, akaandika wimbo, halafu ukimwacha, angeanda apate kulewa. Hatimaye, alimwita mtumishi wake akachukua wembe na kujiua.

48 Watu hawajui yale watu wanaoishi kwenye mazingira ya kiroho wanayopitia. Sasa hapa, unajisikia kana kwamba

ungeweza kuuhamisha mlima, bali acha tu huo upako ukuache, kisha uanze kutokea pale mlangoni . . . Kama mtu fulani hayuko pale kukushika . . . Unaona? Halafu basi, labda kwa saa chache ni vigumu kujua, unashangaa uko wapi. Halafu usiku baada ya usiku, hilo linakumaliza kabisa.

⁴⁹ Na maskini . . . Ninataka kuwaambia kuhusu maskini Sara na Rebeka. Kwa hiyo kesho yake asubuhi, nisingeweza kulala, ndipo nikaamka, nilikuwa nimeketi kitini, na baada ya kitambo kidogo Becky, kwa kuwa ndiye mwenye umri mkubwa zaidi, alikuwa—alikuwa na miguu mirefu kuliko ya Sara, na kwa hiyo Becky akaja mbio . . . akaamka, akaruka kutoka kitandani, pasipo kumwamsha maskini dada yake, naye huyu hapa anakuja katikati ya nyumba, akikimbia upesi awezavyo. Alikuwa akisema, “Baba, Baba . . .” Nikausukuma mbele mmoja wa miguu yangu, naye akaurukia pale, akakaa vizuri kabisa. Kidogo kama ka—kanisa la kisasa, mwajua, limekuwa uwanjani kwa muda mrefu, mwajua, kwa miaka mia kadhaa. Angeweza kujikalisha vizuri sana, kisha akanikumbatia na kusema, “Loo, Baba yangu, Baba yangu . . .”

⁵⁰ Basi maskini Sara alikuwa, katika vurugu hizo, akaamka. Vema, sijui kama watoto wenu hawafanyi hivyo; wangu hufanya: yule mdogo hurithi vazi la mkubwa wake. Na kwa hiyo Sara alikuwa amevaa pajama ya Becky, miguu yake ikiwa mirefu zaidi kiasi hiki, mwajua. Naye huyu hapa anakuja, maskini jamaa mfupi, akianguka, akikikwaa. Basi akafika hapo, kidogo amechelewa. Kwa hiyo Becky akageuka, kasema, “Sara, dadangu, nataka kukwambia jambo fulani.” Akasema, “Nilikuwa wa kwanza hapa. Nami nina uhodhi. Kwa hiyo ninaye Baba wote wala hamna kilichosalia kwako.”

⁵¹ Hivyo ndivyo watu wengine wanavyojaribu kuwazia juu ya dini, siyo? A-ha. Hiyo ni kweli.

⁵² Basi maskini Sara, aliinamisha mdomo wake mdogo, nayo macho yake meusi yakaniangalia, akaangua kilio. Naye Becky alikuwa ameweka shavu lake kwenye langu, akinikumbatia. Ninampenda. Ndipo Sara akaanza kuondoka maana Becky alikuwa na Baba mzima. Nilichomoa goti hilo lingine namna *hii* na kumwashiria namna *hiyo*. Loo, alichangamka mara moja na kutimua mbio, akarukia goti langu ninii sana . . . Hakuwa ameishi muda mrefu sana wala miguu yake hata isingefikia sakafuni. Kwa namna fulani alikuwa kidogo anapepesuka (labda, kama mimi, kupepesuka tu kidogo, mwajua), wala hakuninii . . . asingefikia sakafuni. Hakuwa dhehebu kubwa, mwajua, kwa hiyo asingeweza kuifikia hiyo sakafu ngumu. Hakuwa ameishi muda mrefu kutosha.

⁵³ Na kwa hiyo, kwa namna fulani alikuwa akipepesuka, ndipo nikamkumbatia kwa mikono yote miwili namna *hii* na kumvuta karibu nami, naye akamemetesha maskini macho hayo madogo

meusi, akamgeukia Rebeka. Akasema, “Rebeka, dadangu,” a—akasema, “huenda ikawa ni kweli una Baba wote, bali nataka ujue jambo moja, Baba ana mimi wote.” Kwa hiyo . . .

⁵⁴ Hiyo ni . . . Bora tu Yeye ana mimi wote. Huenda nisiwe na elimu ya kuweka mambo makuu kule, bali pindi tu ninajua Yeye ana mimi wote, katika kupepesuka kwangu, acha tu anikumbatie kwa mikono yote miwili, itanifanya tu nijisikie vizuri.

⁵⁵ Vema, hebu tufanye maombi mengine madogo Kwake kabla ya kulifungua Neno.

⁵⁶ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunatambua ya kwamba sisi ni kama tu watoto pia. Na—Nawe unapenda kuwa pamoja nasi, na kuabudu pamoja nasi. Na tunapokuabudu, na Wewe unatupenda, na kutushika katika mikono Yako, na kumshusha Roho Wako Mtakatifu, na kutufanya tujue ya kwamba Wewe u hai na Wewe ni Baba yetu, tunakushukuru sana. Sasa, jalia Roho Mtakatifu aje kwetu usiku wa leo. Upende kila moyo, Bwana. Tupe baraka mpya. Tumwagie matone ya umande wa rehema, Baba. Usiziangalie dhambi zetu. Ni nyingi mno. Bwana, zisamehe tu. Ziondolee mbali, Baba, na utuchukue tu mikononi Mwako, na—na uyaponye magonjwa yetu, na—na uzisafishe nafsi zetu, na uziweke roho zetu huru, Bwana, tupate kukuabudu na kukusifu, tuwe kama watoto wachanga wanaokimbia huku na huku nyumbani, tukijua tu ya kwamba Baba anatuangalia. Tujalie, Bwana.

⁵⁷ Sasa, hakuna mtu awezaye ku—kulifasiri Neno. Tunatambua hilo. Yohana alikiona kile Kitabu kwenye mkono wa kuume Wake Yeye aliyeketi kwenye kiti cha enzi, na hapakuwapo na mtu mbinguni, wala duniani, wala chini ya ardhi aliyestahili kukitwaa kile Kitabu na kukifungua, ama kuifungua mihuri yake. Ndipo akaja Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naye alistahili. Naye akakitwaa kile Kitabu, kisha akaifungua mihuri, na kukifungua Kitabu. Ee Mwana-Kondoo, njoo usiku wa leo. Tufungulie Kitabu hiki, Baba, tunapokungojea, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwana-Kondoo wa Mungu. Amina.

⁵⁸ Nimechagua usiku wa leo, kifungu kidogo cha Maandiko hapa cha maneno matatu. Lakini kwanza ninataka kusoma kifungu kimoja ama viwili kutoka katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 11 kuanzia kifungu cha 23.

Yesu akamwambia, Ndugu yako atafufuka.

Martha akamwambia, Najua . . . atafufuka tena katika ufufuo siku ya mwisho.

Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi;

Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele, Je! Unayasadiki hayo?

Akamwambia, Naam, Bwana, mimi nimesadiki ya kwamba wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, yule ajaye ulimwenguni.

⁵⁹ Na kwa fungu la maneno ninataka kutumia maneno haya matatu: *Je! Unasadiki Hayo?*

⁶⁰ Nilisoma hadithi fulani wakati fulani uliopita. Nafikiri ilikuwa ni hadithi ya kubuni. Na karibu wahudumu wote, nadhani, wamesoma kitabu cha Dk. Ingraham cha—cha *Mtawala Wa Nyumba Ya Daudi*. Ni kitabu kizuri sana. Ni ninii, nadhani hakipatikani kabisa. Ningetaka kichapishwe, kusudi nikiweke miongoni mwa watu.

⁶¹ Na mle ndani, nilikuwa nikisoma makala kidogo juu ya huyu Lazaro, na juu ya Yesu, na Mariamu, na Martha, kwamba, wale dada zake Lazaro. Nami nilikuwa nikisoma mle ndani kwamba ndiko Yesu aliishi, ninaamini, pamoja na Martha na Mariamu. Wote wawili walikuwa ni wasichana wa kupendeza wa Kiebrania. Naye Lazaro alikuwa akisoma ama kujifunza awe mwandishi hekaluni, kuandika barua za torati kwa ajili ya makuhani.

⁶² Naye Yesu alikuwa na ushirika mkuu sana, hasa sana na Lazaro. Tunaposoma kwenye kitabu hicho kwamba Yeye alikuja nyumbani mwao, naye Martha kidogo akizembea kuhusu kusikiliza maneno Yake, lakini ilimbidi kuandaa chakula cha jioni na kuandaa meza, bali Mariamu aliketi miguuni Pake. Naye Yesu alisema kwamba Mariamu amechagua mambo yaliyo bora.

⁶³ Halafu basi, tuliambiwa ya kwamba Lazaro ndiye aliyemleta Yesu kwa Yohana, katika hadithi ya vitabu vya Dk. Ingraham, na...kwenye *Mtawala Wa Nyumba Ya Daudi*. Hata hivyo, huenda hiyo haikuwa ni kweli, sijui mimi, bali kwa ajili tu ya msingi wake, ila alidhaniwa kwamba alikuwa akiishi pamoja nao.

⁶⁴ Sasa, tumekuwa tukisoma juma hili lijalo, hili lililopita, hasa, ya kwamba Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Mimi...Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda: ndilo analotenda Mwana vile vile. Baba anatenda kazi Naye Mwana anatenda kazi.” Mnaona? “Yale anayomwona Baba akitenda.”

⁶⁵ Kwa hiyo kuifanya hii hadithi ya kweli kabisa, Baba, Mungu, hapana budi alinena na Mwanawe, Yesu, na kusema, “Rafiki Yako, Lazaro, atakufa, bali itakuwa ni kwa manufaa, kwa hiyo Wewe ondoka nyumbani. Nenda mbali, kwa kuwa watakusihi kumwomba, ama, kumponya, na—na Mimi sitaki ufanye hivyo.” Kama utaiangalia hadithi hii tunapoendelea, utaona ikilundikana kwenye ukweli wa jambo hilo. Kwa hiyo, Yesu, pasipo ilani yoyote wala chochote kile, aliondoka nyumbani

akaenda mahali pengine, hakurudi usiku huo. Basi akaenda kwenye miji mingine. Na mara Yesu alipoondoka nyumbani, basi shida ikaingia.

⁶⁶ Na wakati Yesu anapoondoka nyumbani mwako, shida iko njiani. Kumbuka tu, anapoondoka nyumbani mwako shida iko njiani. Unaporuhusu mashirika ya umma na kadhalika kuendeshwa kikamilifu kanisani mwako, kama Rikenibaka kubwa mno ya silinda kumi na sita, nanyi hamumhusishi Yesu, Yesu anapoondoka kanisani mwenu, shida iko njiani. Naam, bwana, Yesu anapoliacha dhehebu, ambao wanamweka kando na kusema, “Vema, sasa hatuamini kabisa kwamba mambo haya yangekuwa ni ya kweli kabisa,” nanyi mnachukua kitu kingine, shida iko njiani. Kumbukeni tu hilo.

⁶⁷ Yanikumbusha juu ya hadithi ya Bwana Yesu, inayopatikana katika Kitabu cha Luka. Mnajua wakati alipokuwa tu ni mvulana wa yapata umri wa miaka kumi na miwili, watu Wake walimpeleka, kama ilivyokuwa desturi kila mwaka, kwenye sikukuu ya Pentekoste. Basi walipokuwa katika mji wa Yerusalemu kwenye karamu hiyo na wakiwa na wakati mzuri, tunaona katika Biblia, ya kwamba walienda siku tatu bila Yeye. Na kwamba wao walidhani labda, walichukulia tu kama ni kweli, ya kwamba hapana budi Yesu alikuwa miongoni mwa baadhi ya jamaa zao. Sasa, hatuwezi kufanya hivyo. Walipopitia kwenye jamaa zao wakimtafuta, Yeye hakuwapo.

⁶⁸ Na sisi hatuwezi kulichukulia kwamba ni kweli, ati kwa sababu tu sisi ni Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, na misingi yetu na babu zetu walikuwa ni waaminio hodari, tunalichukulia tu, vema, kwamba ni kweli, Yesu yu pamoja nasi. Hatuwezi kufanya hivyo. Inatupasa kuwasiliana Naye kila siku na kila dakika. Loo, ninapenda hilo.

⁶⁹ Nataka kile Mungu alichosasa. Kile wazazi wangu walichokuwa nacho, kile babu zangu walichokuwa nacho, ni kizuri sana. Lakini kile walichokuwa nacho ni kizuri. Nafikiri tumesonga mbele zaidi.

⁷⁰ Hebu tuone kile alicholeo leo hii. Sitaki kuangalia nyuma na kuona kile Bw. Moody alichofanya, kwa kuwa tuko mbali zaidi njiani kuliko Bw. Moody. Shida ya makanisa yetu tunaangalia nyuma na kusema, “Vema, hebu tuone kile Bw. John Wesley alichosema, kile baadhi ya hao wengine walichosema.” Hiyo ndiyo sababu sayansi iko mbali zaidi kwenye fani zao, kuliko dini ilivyo kwenye zake.

⁷¹ Hapa miaka mia tatu iliyopita, mwanasayansi Mfaransa alithibitisha ya kwamba kama ungeenda kwa mwendo wa kasi mno wa maili thelathini na tano kwa saa, uvutano ungekuondoa ardhini. Mnafikiri sayansi ingerejea kwenye hilo leo hii? Wanaenda maili elfu moja mia tisa kwa saa na wangali wanaendelea. Wanakaza mwendo kwenda mbele, wakiangalia

mbele. Lakini sisi tunataka kuangalia nyuma na kuona yale Moody aliyosema; aliyosema Sankey; aliyosema Finney; Knox, Calvin; baadhi ya hao. Waliyosema yalikuwa ni sawa. Hayo yalikuwa ni kwa ajili ya wakati wao, bali sisi tunasonga mbele.

⁷² Babu yangu alipanda mkokoteni wa maksai. Ninaendesha Ford V8. Mwanangu ataruka kwa ndege. Hiyo ni kusema, tunasonga mbele. Hivyo ndivyo dini inavyopaswa kuwa. Kuja kwa Bwana kumekaribia. Kanisa linapaswa kuwa likiingia kwenye mamlaka yake. Sayansi inaweza tu kupanda hadi kiwango fulani, kisha haina budi kushuka, bali sisi tuna rasilimali zisizotumika bado, ambazo hazijapata kuguswa, za nguvu, zisizo na kikomo, za Mungu, tunazopaswa kuwa tukiziendea. Tunaishi maili milioni moja chini ya majaliwa yetu usiku wa leo, majaliwa ambayo Wakristo wanapaswa kuwa wakifurahia. Ninajionea aibu ninapotazama hapa nje na kuona taasisi, na magonjwa, na shida zinazoendelea sasa hivi. Kanisa letu linapaswa kuwa likitembea mtaani, likiwaponya wagonjwa, likiwafufua wafu, likiwatoa pepo, kufanya ishara na maajabu, likiufanya ulimwengu mzima utambue ya kwamba Yesu yu hai. Hayo ndiyo tunayopaswa kuwa tukiyafanya.

⁷³ Mbona, unasema, “Bw. Moody kamwe...” Bw. Moody hakuwa akiishi leo hii. Hiyo ni kweli. Tunaishi kwenye kule kuja kwa Bwana. Nasi tumelichukulia tu kwamba ni kweli kwamba alikuwa pamoja na jamaa zetu. Lakini hivi majuzi mpinzani alipompa Bw. Graham changamoto, tulikuta kwamba Yeye hakuwa miongoni mwa jamaa zetu.

⁷⁴ Wanampata wapi? Ni wapi—ni wapi walipompata Yesu? Pale pale walipomwacha. Walimwacha wapi? Kwenye karamu ya Pentekoste. Tunamwacha Yesu wapi, kanisa lilimwacha wapi? Kwenye karamu ya Pentekoste. Tunapoondoka kwenye zile nguvu za kale za Pentekoste na karamu ya Pentekoste, tunamwacha Yesu. Hiyo ni kweli kabisa, rafiki. Tumepoteza haki zetu. Naam, bwana.

⁷⁵ Walimwacha kwenye sikukuu ya Pentekoste, na hapo ndipo mahali pekee ambapo Methodist, Baptisti, Presbiteri, na Wapentekoste watakapompata, ni kurudi mahali walipomwacha. Furaha ya Bwana iko wapi? Nguvu za Bwana ziko wapi? Kanisa linauliza leo hii, “Ni nini—ni nini kilichompata Mungu wa historia?” Yeye anawangojea watu Wake wamwite jukwaani. Lakini ninii...

⁷⁶ Hatuwezi kufanya hivyo kupitia madhehebu. Hatuwezi kufanya hivyo chini ya saikolojia. Hatuwezi kufanya hivyo chini ya hisabati, wala hatuwezi kufanya hivyo kwa elimu. Tunajitenga, tunajigawanya. Hatujagawanyika. Sisi kweli ni mtu mmoja katika Kristo Yesu. Sisi sote ni mmoja katika Kristo, wala madhehebu yetu hayatafaulu. Ingawa ni mazuri

sana, hayatafaulu. Elimu yetu ndiyo kizuizi kikuu sana Injili ilichopata kuwa nacho, ni elimu.

⁷⁷ Tunachohitaji si elimu. Tunahitaji nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu yarudishwe kanisani kuzidhihirisha zile nguvu. Yesu kamwe hakusema, “Enendeni ulimwenguni kote na—na kufundisha.” Kamwe hakusema, “Enendeni ulimwenguni kote na kufanya...” Alisema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili.” Nayo Injili ni kudhihirisha nguvu za Roho Mtakatifu, ufufuo. Tungali umbali wa maili milioni moja kutoka mahali tunapopaswa kuwa. Hebu tusonge mbele. Na turudi tulipomwacha kwenye karamu ya Pentekoste.

⁷⁸ Yesu alisema, katika Yohana, ninaamini, mlango wa 15, alisema, “Mimi Ndimi Mzabibu; ninyi ni matawi.” Vema sasa, kama huo Mzabibu ulizaa tawi la kwanza, na kutokana na tawi hilo kikaandikwa Kitabu cha Matendo, tawi la pili litafanya Kitabu kingine cha Matendo. Tawi la tatu litafanya Kitabu kingine cha Matendo. Na kila tawi linalotokana na Mzabibu huo litakuwa kama lile tawi la kwanza lilivyokuwa.

⁷⁹ Sasa, unaweza ukapandikiza, tunajua hilo. Nimeona mti wa aina ya mchungwa ukiwa na matunda aina nane mbalimbali. Nimeona mchungwa ukizaa mibalungi, na malimau, na chochote kingine juu yake, bali yalikuwa yamepandikizwa.

⁸⁰ Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Tumepandikiza mawazo yetu, tukapandikiza madhehebu yetu, bali kama mti huo ukitoa tawi lingine la tunda, wenyewe, litakuwa kama yale ya asili yaliyoingia kwake. Haleluya! Loo, kanisa litaungana pamoja, bali tunahitaji nguvu za ule wa asili. Tunahitaji Roho Mtakatifu, zile nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo. Hivyo ndivyo alivyotwambia tufanye.

⁸¹ “Mimi Ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi.” Kama mzabibu ukizaa tawi, nalo linatokea na zabibu nzuri za bluu, tawi la pili utakalozaa litakuwa na zabibu nzuri za bluu. Kama Mzabibu wa kwanza ulijitokeza, nao wakaanguka chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, nao wakafanya miujiza mikuu, na ishara, na kutia muhuri ushuhuda wao kwa ulimwengu... Hata wengi wao wakiwa na ushuhuda wao wenyewe, wao, kwa damu yao, walitia muhuri ushuhuda wao. Walipitia kwenye kila namna ya hatari na kadhalika kuileta Injili. Waliteseka, walipigwa; waliadhibiwa. “Yatubidi kupelekwa nyumbani Mbinguni juu ya kitanda cha maua ya raha, wakati wengine walipiga vita wakashinde tuzo, na kuabiri kwenye bahari zenye damu?” Tunatarajia kufanya nini? “Sharti nipigane kama inanibidi kutawala. Niongezee ushujaa, Bwana.” Hakika. Tunahitaji...

⁸² Hatuhitaji dhehebu jipya. Hatuhitaji jengo jipya la kanisa. Tunachohitaji leo hii ni uamsho wa Kipentekoste wa mtindo wa kale wa huko nyuma misituni, wa mbingu za bluu, unaongamiza

dhambi, uliozaliwa pale Pentekoste na umerudi kanisani tena, nguvu za Roho Mtakatifu tena, kumleta Yesu jukwaani.

⁸³ Mungu wa historia daima hujitokeza jukwaani wakati muhimu. Tunahitaji hilo. Hiyo ndiyo shida ya kanisa letu leo hii. Tunarudi nyuma mno. Tunavutiwa na mitindo ya ulimwengu. Na polepole, mwaka baada ya mwaka, linaanza kufa kidogo na kunyauka.

⁸⁴ Ni wakati wa kupogolewa hivi karibuni sana. Mungu atalikatilia mbali hakika tu kama ninavyosimama kwenye mimbara hii. Mungu atalipogoa lipate kuzaa tunda. Ataukata aondoe matendo ya ulimwengu moja ya siku hizi. Ni fedheha jinsi gani, jinsi kanisa limejiendeleza chini ya jina la dini.

⁸⁵ Nasi tunaona, wakati Yesu alipoondoka, mauti yaliingia. Yesu anapoondoka kanisani mwetu, nguvu za Roho Mtakatifu zinaondoka kanisani mwetu, linaanza kufifia na—na kufa. Na baada ya kitambo kidogo halina kitu. Sasa, Yesu alipoondoka, mauti yaliingia. Loo, jinsi ulivyokuwa ni wakati wa huzuni.

⁸⁶ Pia angalieni, walishikwa na mshangao, kisha wakaagiza Yesu aitwe, bali hakuja. Wakaagiza tena aitwe, bali Yeye hakuja, ila alijua kile atakachofanya. Yeye anajua usiku wa leo, kile atakachofanya. Hajasahau: anajua kile hasa anachotaka kufanya. Atawainua watu, hakika tu kama ninavyosimama kwenye mimbara hii. Atawainua watu kwa ajili ya Jina Lake kutoka kwenye kizazi cha Mataifa. Atawainua.

⁸⁷ Ni wakati wa Wayahudi umekaribia sana sasa, nao wa Mataifa unakwisha, kwa sababu wao walitoka tu. Wanamkataa Kristo; wanazikataa ishara zao; wanakataa kila kitu kinachoitwa utaua, na kukiita namna fulani ya kusoma mawazo ama nguvu za ibilisi na kuninii. . . Wanamkufuru Roho Mtakatifu na kujitia muhuri mbali na Mungu. Naye Mungu atawachukua hao walio wachache, baada ya kitambo kidogo, na kuwainua wakawa Kanisa lenye nguvu, kisha amrudishe Roho kwa Wayahudi, na kulipeleka Kanisa la Kimataifa nyumbani. Kweli kabisa. Linajiandaa sasa. Loo, jinsi, tuko kwenye wakati wa mwisho, karibu.

⁸⁸ Yesu, Yeye alijua. Na baada ya kitambo kidogo Yeye alisema, “Rafiki yetu, Lazaro, amelala.”

⁸⁹ Mbona, hao wanafunzi walifikiri alikuwa akipumzika kidogo. Akasema, “Vema, ikiwa amelala, anafanya vema.”

⁹⁰ Vema, alisema katika ninii Yake. . . maneno yao, kusudi wapate kuelewa, kasema, “Amekufa, na kwa ajili yenu nafurahi kwamba sikuwako.” Mnaona? “Kwa ajili yenu, nafurahi kwamba sikuwako.” Kwa maana wangekuwa wakimsihi a—amponye—amponye, bali Yeye alijua asingefanya hivyo, kwa kuwa hilo ono lilikuwa bado. . . baada ya siku hizo nne alijua huo ulikuwa ndio wakati Baba alikuwa amemwambia. Ni la kupendeza jinsi gani; Yeye alisema pale kaburini, “Baba, nakushukuru,

umesikia tayari, bali ninasema hivi tu kwa ajili ya hawa wanaosimama hapa.” Mnaona? Yeye tayari alijua atakalofanya. Alisema, “Ninakwenda kumwamsha.”

⁹¹ Sasa, naweza kuwazia maskini makazi hayo yalikuwa yamehuzunika sana. Mkimu familia alikuwa amewaacha, huzuni. Loo, ni furaha sana unapokuwa na makazi yenye huzuni ama moyo wenye huzuni, halafu Yesu anatokea mara moja, sivyo? Ninaweza kuwazia kumwona Martha, maskini msichana mrembo mwenye shela jeusi juu ya uso wake, na maskini Mariamu, nao wameshikana, wakisema, “Tutafanya nini? Baba na Mama wameondoka, na ndugu yetu mpendwa . . . Sasa, tumeondoka kanisani, nasi tumefukuzwa kutoka kwao, na tukatoka kuja kumfuata Yesu wa Nazareti. Naye ameondoka na kutuacha, mahali fulani.”

⁹² Ninaweza kumsikia mkosoaji akija pale na kusema, “Aisee, yuko wapi yule Mponyaji wa Kiungu, yule Nabii wa Galilaya? Yuko wapi sasa? Mnaona, inapofikia hasa kwenye wakati Wake wa kufanya jambo, ameondoka.” Haya basi. Mnaona, Mungu anapenda tu kufanya jambo hilo, kuwaacha tu watu, ninii tu, kuwaacha watu waonyeshe jinsi walivyo, naam, akiwajaribu tu apate kuona jinsi walivyo hasa. Yeye huwapa baraka. Anaonekana, anajionyesha, anajitambulisha Mwenyewe kwa watu, apate kuona tu watachukua msimamo gani, apate tu kuona kile watakachofanya juu yake.

⁹³ Sasa, tunaona basi, baada ya—ya siku chache, siku nne, maskini Lazaro alikuwa amekufa. Wakamzika. Siku ya pili, siku ya tatu, siku ya nne . . . Sasa, kila mtu anajua uharibifu huingia baada ya siku tatu: pua inatumbukia usoni, kwanza. Kisha uharibifu unaingia; mabuu ya ngozi yanaanza kuula mwili. Wakamlaza chini, wakaweka mwamba mkubwa juu ya lile pango walipomlaza. Na mara kwa mara, hao wasichana wadogo wangetoka na kupiga magoti hapo kaburini na kulia.

⁹⁴ Na baada ya muda mfupi, habari zikaenea, “Yesu amekuja. Tulimwona akiingia mjini.” Loo, maskini yule Martha, aliyekuwa ameninii sana, ilivyoonekana, amezembea sana kulihusu, alithibitisha basi kile alichokuwa. Huyu hapa anakuja. Yuko njiani basi, anakimbia akitafuta. Ninaweza kuwasikia baadhi yao barabarani wakisema, “Vema, nadhani umeridhika sasa, kwamba dini yenu ilikuwa ni ya uongo.” Aliwapuza tu na kuenda zake, akawapita wakosoaji wote. Alishuka mpaka akamwona, labda ameketi pembeni mwa mtaa.

⁹⁵ Sasa, ilionekana, hapana budi yeye . . . huenda alikuwa na haki ya kumkemea na—na kumkena vibaya. Mbona, yeye hakukimbia kule na kusema, “Angalia hapa, angalia hapa, Wewe. Unadhaniwa kwamba u Nabii, Mtu wa Mungu. Mbona hukuja tulipokuita? Mbona, tumekuwa ndio kitu cha kuchekwa mjini sasa. Tulitoka kanisani mwetu tupate kukufuata.”

Ilionekana kana kwamba alikuwa na haki. Lakini mnajua, kama tu vile nilivyohubiri juu ya, *Mwana-Kondoo Na Hua*, ikiwa sisi ni mwana-kondoo, mwana-kondoo hupoteza kila haki aliyo nayo. Ni kweli kabisa. Hana kitu ila sufu, kwa hiyo hana budi kuipoteza hiyo. Nawe unapoteza kila haki uliyo nayo upate kumtumikia Mungu. Hiyo ni kweli kabisa.

⁹⁶ Nilikuwa nikiwakemea wanawake kuhusu jinsi walivyokuwa wakivaa maskini nguo hizi fupi, mwajua, nao wakasema, “Vema, sisi—sisi ni Wamarekani. Tunaweza kufanya tutakacho.”

⁹⁷ Nikasema, “Hiyo ni kweli kabisa, bali kama wewe ni mwana-kondoo, utapoteza haki zako.” Kuvuta sigara na kufanya vituko namna hiyo, hilo ndilo jambo baya sana mwanamke alipata kufanya. Hiyo ni kweli kabisa.

⁹⁸ Mama fulani aliniambia, si muda mrefu uliopita, akiongea nami, kasema, “Lakini, Ndugu Branham, hawatengenezi nguo za aina nyingine tofauti.”

⁹⁹ Nikasema, “Lakini wangali wanatengeneza cherahani na kuuza vitambaa. Hakuna udhuru kwa hilo hata kidogo.” Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁰⁰ Kumbukeni, siku moja, huenda ukawa safi hapa kwa mume wako, bali utawajibika kwa uzinzi kwa jambo hilo, hakika: “Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.”

¹⁰¹ Wanawake wa Kipentekoste wana shida gani siku hizi, ndilo ninalojiuliza. Jinsi mmeondoka kwenye uaminifu wa kale. Jinsi mama zenu walikuwa na nywele ndefu, na leo hii wanawake Wapentekoste wanajipodaa kama kundi la Wavaa Vinyago, na kukata nywele zao, na kuvaa maskini nguo fupi namna hiyo, kama tu wengine wao. . . wanatoka na kukata nyasi alasiri, wakati wanaume wanapitapita, hivi unatambua, ewe mwanamke, ya kwamba itakubidi kuwajibika kwa kuzini na hao wanaume? Unajianika kwao kwa kusudi hilo. Ni pepo mchafu juu ya kanisa pamoja na watu, wala hawajui. Vipofu wala hawajui. Ni kweli.

¹⁰² Labda mtasema sina haki ya kusema hivyo kama mwinjilisti. Vema, si—sina budi kuufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu; hayo tu ndiyo ninayoweza kusema. Ninyi. . . Kama nikikutana nanyi kwenye hukumu, basi haitanibidi kuwa na damu yenu mikononi mwangu. Ondoka kwenye kila eneo linaloonekana kama Shetani. Kaa mbali. Ondoka humo. Sijali ni nyota wangapi wa televisheni. . . Wewe huko hapa, kama nyota wa televisheni; wewe ni binti ya Mungu.

¹⁰³ Nilihubiri kwenye kanisa la mchungaji mmoja hivi majuzi asubuhi, kuhusu maskini mtumwa, wakati walipokuwa wakiwauza watumwa zamani za kale. Nao walikuwa wakija na kuwanunua kwenye mnada. Nao hao watu walikuwa,

walikuwa wanalia, kuomboleza, kwa sababu ya nchi ya uenyeji wao; hawatarudi tena. Nao iliwabidi kuwapiga mijeledi. Nao wangewanunua kama tu vile ungenunua gari, rahisi sana, bei zao, na kuwauza hao wanadamu.

¹⁰⁴ Basi siku moja, mnunuzi alikuja, dalali, kwenye ninii kubwa...shamba kubwa, hasa. Na akasema, “Una watumwa wangapi wa kuuzwa?”

¹⁰⁵ Kasema, “Vema, nina wachache wa kubadilishana.” Wangejaribu kuwatafuta walio wakubwa. Wanawachukua hao akina mama, baba...Kama alikuwa amemwoa mwanamke mdogo na dhaifu, wanawachukua hawa wanaume wakubwa wenye afya na kuwazalisha kwa...kama farasi na wanyama. Haijapata kuwa halali kamwe. Mungu alimuumba mwanadamu. Mwanadamu akawafanya watumwa. Si halali, kamwe. Mungu hamkusudii mtu yeyote kuwa mtumwa. La, bwana. Pia hakuna...Angalia kilichotukia.

¹⁰⁶ Ndipo katikati ya hayo yote, jamaa huyu akasema, “Vema, ningetaka kununua baadhi yao...” Akamwona jamaa mmoja mdogo pale. Haikuwabidi kumcharaza. Alikuwa ameinua kidevu chake, kichwa kimeinuliwa, kama tu muungwana, akitembea huku na huku. Ndipo huyo dalali akasema, “Nitamnunua.”

¹⁰⁷ Akasema, “Lakini yeye hauzwi.”

¹⁰⁸ Akasema, “Vema, kwa nini?” Kasema, “Kwani yeye ndiye bosi?”

¹⁰⁹ Akasema, “Hasha, ni mtumwa.”

¹¹⁰ “Vema,” kasema, “mbona? Hivi unamlisha vizuri kuliko unavyowalisha hao wengine?”

¹¹¹ Akasema, “La. Yeye hula pale nje manchani pamoja na hao wengine. Yeye ni mtumwa.”

¹¹² Kasema, “Ni kitu gani kinachomfanya kuwa tofauti sana na wenzake?”

¹¹³ Basi huyo bosi akasema, “Nilishangaa vivyo hivyo mimi kwa muda mrefu, lakini siku moja nikagundua. Huko kwenye nchi ya uenyeji, baba yake ndiye mfalme wa kabila lao. Na ingawa yeye ni mgeni mbali na nyumbani, angali anajua yeye ni mwana wa mfalme na anatenda kama mmoja.” Kama hiyo...Kama Mwafrika asili anaweza kutambua ya kwamba baba yake ni mfalme, na huku akiwa ni mgeni katika nchi ya kigeni angali anaweza kujua ya kwamba ng'ambo ya bahari yeye ni mwana wa mfalme, inapasaje wanawake na wanaume kujitendekeza wakati ninyi ni wana na binti za Mungu? Tendeni kama hao. Hakika. Tendeni; jisafisheni na kutenda kama wana na binti za Mungu. Si ajabu, ni hali ya jinsi gani.

¹¹⁴ Sisi hapa. Loo, maskini Martha, akaja mbio. Ilionekana kana kwamba alikuwa na nji—njia ya kusema jambo dhidi

Yake. “Kwa nini hukuja kwa ndugu yangu? Angalia yale tumekufanyia, Nawe ukatuaibisha.” Vema, kama angalisema hivyo, hiyo hadithi kamwe isingaliishia jinsi ilivyoishia. La, bwana. Ni vile unavyoiendea karama ya Kiungu ya Mungu. Kama Mungu akituma karama, inakupasa kuiendea vizuri. Iwapo kwa vyovyote unataka kupata kitu kutoka kwake, huna budi kuiendea vizuri. Naye Martha alijua hivyo. Huenda alikuwa amesoma kuhusu yule mwanamke Mshunani na mtoto wake mchanga. Naye. . . Kama mwanamke huyo Mshunani alijua ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya Eliya, ni zaidi sana jinsi gani alivyokuwa ndani ya Yesu? Hakika.

¹¹⁵ Kwa hiyo, alipanda akaenda na mtazamo mzuri. Alikimbia na kuanguka miguuni Pake. Ninapenda hilo! Akaanguka miguuni Pake na kusema, “Bwana. . .” Hicho ndicho cheo Chake sahihi. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Alikuwa ni Bwana wake. “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.”

¹¹⁶ Loo, jamani. Loo, ninaweza tu kuwazia nikiuona moyo Wake mkuu wakati akimwangalia msichana huyo mrembo, machozi yakitiririka mashavuni mwake. Kasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.” Angalia yale aliyosema. “Lakini hata sasa, Bwana, ingawa amekufa, ingawa mabuu ya ngozi yanatambaa mwilini mwake, hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

¹¹⁷ Loo, hiyo ndiyo siri. Huenda ukasema, “Nimepitia kwenye kila hospitali. Daktari anasema nitakufa, lakini hata sasa, Bwana. . . Nimelemaa kabisa kwa yabisi kavu; siwezi kusogea, lakini hata sasa, Bwana. . .”

¹¹⁸ Maskini mtoto yule mchanga alikuwa na kichwa kilichojawa maji kikubwa hivi jana usiku. Hakuna kitu unachoweza kufanya. Yangeenea na kukipasua maskini kichwa chake na kufa, “Lakini hata sasa, Bwana. . .” Angali ni Mungu yeye yule. Angali ni Bwana yeye yule. “Hata sasa, Bwana. . .” Naye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Mwenyezi Mungu, akiombea mambo ambayo tunadai kwamba ametufanyia.

¹¹⁹ Sasa, kweli ninajisikia wa kidini. Hakika najisikia. Mtaniita mtakatifu anayejifingirisha kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali muanze, mkatosheke nayo.

¹²⁰ Kwa hiyo, naam, bwana, “Hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya.”

¹²¹ “Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya,” Yesu alisema.

¹²² “Hata sasa, Bwana, lolote utakaloomba, Mungu atakupa.” Loo, hilo hapana budi liliuchochea moyo Wake mkuu.

¹²³ Akasema, “Ndugu yako ataishi tena.”

¹²⁴ Akasema, “Naam, Bwana. Ataishi. Alikuwa ni mvulana mzuri. Atafufuka katika ufufuo wa kiama katika siku ya

mwisho.” Hao Wayahudi waliamini katika ufufuo wa kiamaa. “Atafufuka katika ufufuo wa siku za mwisho.”

¹²⁵ Mwangalieni. Aliukusanya maskini mwili Wake pamoja. Akasema, “Mimi Ndimi Ufufuo na Uzima.” Loo, jamani. Hakukuwahi kuwako na mtu angaliweza kusema hivyo hapo kabla. Kamwe hapatakuwapo na mwingine baadaye, anayeweza kulisema. Yeye Ndiye tu anayeweza kulisema. “Mimi Ndimi Ufufuo na Uzima,” asema Bwana. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Naye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Je! Unasadiki hayo?”

¹²⁶ Akasema, “Naam, Bwana.” Loo, alijua kitu fulani kilikuwa karibu kutukia. Hakina budi.

¹²⁷ Wakati imani kutoka kwenye moyo mwaminifu inapokutana na Mungu, basi hayo meno ya magurudumu yanaumana namna *hiyo*. Jambo fulani halina budi kutukia. Ninawapa changamoto wasikilizaji hawa usiku wa leo, katika Jina la Yesu Kristo, hebu imani yenu iungane na Mungu namna hiyo, katika dakika chache tutakuwa na Pentekoste nyingine. Kutakuwako na uamsho mkuu sana utakaoibuka katika mji huu, kusingekuwako na polisi wa kutosha nchini kuwakomesha. Hiyo ni kweli. Kutakuwako na uamsho halisi. “Hata sasa, Bwana . . .”

¹²⁸ “Vema, Bwana, tayari tumeshika hili; tumefanya hili na kufanya lile.” Sijali umefanya nini, “Hata sasa, Bwana . . .” Yeye anawangojea kumwita. Yeye . . . “Je! Unasadiki hayo?” Hakika. Naam, bwana. Hata sasa, lolote utakalomwomba . . .

¹²⁹ “Mmemlaza wapi?” Sasa, anashuka kwenda kaburini. Alikuwa mwanadamu kutosha kulia; alikuwa Mungu kutosha kufufua wafu.

¹³⁰ Hapa wakati fulani uliopita, mwanamke ambaye ni mwanachama wa kundi fulani la watu . . . Kamwe sijzoeshi kuyaanika madhehebu. Lakini mwanamke huyu . . . Hao hawaamini ya kwamba Yesu alikuwa ni wa Kiungu. Walisema Yeye alikuwa tu ni nabii. Sasa, Yeye alikuwa . . . Kama alikuwa nabii tu, sote tumo katika dhambi. Ama alikuwa ni Mungu, si kitu pungufu ya Mungu, au mdanganyifu mkubwa sana ulimwengu uliopata kuwa naye. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Akasema, “Hakuwa wa Kiungu.”

¹³¹ Kuna mengi sana ya hayo katika injili hii ya umma leo hii; kujaribu kumfanya Yesu Kristo nabii. Mbona, Yeye alikuwa Mungu wa manabii. Hakika alikuwa hivyo.

¹³² Akasema, “Nitakuthibitishia kwa Biblia yako, ‘Alikuwa tu ni mwanadamu.’”

¹³³ Nikasema, “Thibitisha.”

¹³⁴ Naye akasema, “Alipoenda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema, ‘Alilia.’ Ilibidi awe mwanadamu la siyo asingeweza kulia.”

135 Nikasema, “Ewe mama, hayo ndiyo Maandiko yako?” Simaanishi kukufuru hapa kusema hili, bali nitawaambia yale niliyomwambia.

136 Akasema, “Hayo ndiyo.”

137 Nikasema, “Tamshi hilo ni dhaifu kuliko mchuzi uliopikwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa.” Nikasema, “Vema, hu—huna hata jambo moja la kusimamia.”

138 Akasema, “Mbona, Yeye alilia. Hiyo ilionyesha Yeye alikuwa ni mwanadamu.”

139 Nikasema, “Yeye alikuwa anayepatikana na mauti na asiyeapatikana na mauti. Alikuwa ni Mungu katika mwili.”

140 Akasema, “Loo, upuuzi huo.”

141 Nikasema, “Alienda kaburini akilia. Hiyo ni kweli vya kutosha, bali wakati alipounyosha maskini mwili Wake...” Biblia ilisema, “Hakuwa na mengi ya kuvutia macho; hana uzuri hata tumtamani.” Lakini wakati alipoyatupa maskini mabega hayo nyuma na kusema, “Lazaro, njoo huku nje,” naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne na kuoza kaburini, akatoka nje. Huyu alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Nionyeshe mtu anayeweza kufanya hilo. Ilikuwa ni kitu gani? Uharibifu ulimjua Bwana wake. Uzima ulimjua Muumba wake. Ilibidi jambo fulani litukie. Alinena na mtu aliyekuwa amekufa na yumo kaburini kwa siku nne, akafufuka tena, na akasimama kwa miguu yake, na kuishi. Haleluya! Huyu alikuwa ni Mungu katika Mwanawe. Naam, bwana. Huyu alikuwa ni Mungu akijitambulisha Kwake, Mwanawe. Huyu alikuwa ni Mungu akinena, sio mwanadamu.

142 Alikuwa mwanadamu wakati alipoangalia kwenye ule mti siku ile apate chakula. Huyu alikuwa ni mwanadamu. Bali hapo alipochukua biskuti tano na samaki wawili na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyu alikuwa ni Mungu akiwalisha mle ndani. Alikuwa ni zaidi ya nabii, zaidi ya mwanadamu, alikuwa ni Mungu-Mtu. Hakika.

143 Alilala nyuma ya ile mashua ndogo usiku huo, huku bahari zikinguruma na kurukaruka kama kifuniko cha chupa huko nje kwenye bahari hiyo yenye nguvu, wakati pepo elfu kumi wa baharini waliapa wangemzamia usiku huo. Alikuwa ni mwanadamu, mnyonge na mchovu kutokana na kuwaombea wagonjwa, amelala pale nyuma; na upepo hata haukumsumbua. Alikuwa ni mwanadamu wakati alipolala usingizi, bali alipoamka, akaweka mguu wake kwenye demani ya mtumbwi huo, akaangalia juu, akasema, “Amani, tulia,” nazo pepo na mawimbi yakamtii, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyu alikuwa ni Mungu katika mwanadamu, akijitambulisha. Hiyo ni kweli.

144 Alikuwa mwanadamu msalabani hapo alipolia apate rehema. Hapo alipolia na kusema, “Naona kiu,” huyo alikuwa

ni mwanadamu. Wakati alipokufa, alikuwa ni mwanadamu, lakini kwenye ile asubuhi ya Pasaka wakati alipovunja mihuri ya mauti, kuzimu na kaburi, na kufufuka tena, Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu: ilikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa. Si ajabu mshairi alisema:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, akaniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja yuaja—Ee, siku yenye utukufu!

¹⁴⁵ Yeye alisema, “Kwa kuwa ni hai, ninyi nanyi mtaishi. Je! mnasadiki hayo?” Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! mnasadiki hayo? Ninaamini Roho Mtakatifu yuko papa hapa sasa. Je! mnasadiki hayo? Ninaamini atatuja kwa Uwepo Wake. Je! mnasadiki hayo? Ninaamini Roho Mtakatifu anataka kutumiminia Uwepo Wake, kuwaponya wagonjwa wote, kuwafanya watu wote wasio na Roho Mtakatifu wajazwe. Je! mnasadiki hayo? Mnasadiki kwa moyo wenu wote? Na tusimame kwa miguu yetu na kumpa sifa. Ninaamini atashuka sasa hivi juu yetu.

¹⁴⁶ Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, Mpaji wa kila kitu chema, sisi “Tunasadiki hayo,” Bwana. Tunasadiki ya kwamba huyo ni Wewe hapa mkutanoni. Tunasadiki ya kwamba huyo ni Wewe unayezibariki nafsi zetu. Tunasadiki ya kwamba huyo ni Wewe unayemimina Roho Wako juu yetu. Tunasadiki ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunasadiki Wewe u hai milele na majina yetu yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Mbingu zote na nchi zitapita, bali sisi tutaishi milele, kwa maana Wewe u hai milele. Bwana, ulituahidi hilo. Tunasadiki kwa moyo wetu wote. Kila kitu kilicho ndani yetu, tunakisadiki, Bwana. Ninampenda, ninampenda.

¹⁴⁷ Je! mnamwamini? Ninaamini huyo ni Roho Mtakatifu. Kuna kitu kinachotuangukia. Je! mnasadiki hayo? Ninasadiki anataka kumponya kila mtu sasa hivi. Je! mnasadiki hayo? Mwinulieni mikono yenu. Simameni kwa miguu yenu. Je! mnasadiki hayo? Roho Mtakatifu yupo hapa. Hili ni Lile! Petro alisema, “Hili ni Lile.” Ndilo hili, Roho Mtakatifu.

¹⁴⁸ Ee Bwana, Muumba wa mbingu na nchi, zitume nguvu Zako, na baraka Zako, na wema Wako juu ya watu hawa, na uibariki mioyo yao, na uwajalie waone kwamba Mwana wa Adamu yu hai milele. Tujalie, Ee Bwana. Tunawaleta Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

¹⁴⁹ Mtu yeyote asiye na Roho Mtakatifu, inua mikono yako na umsifu Mungu. Ninaamini atakujaza. Mtu fulani awawekee mikono. Hii ndiyo saa. Kwa nini tungoje zaidi? Huu ndio wakati. Huu ndio wakati wa Pentekoste, kumrudia Mungu. Jiweke sawa na Mungu, Pentekoste! Hebu moyo wako uchochewe na nguvu

za Mungu aliye hai. Hebu Roho Wake aje aingie ndani yenu, akijaza kabisa nafsi zenu. Yeye yupo hapa usiku baada ya usiku, hapa kuwaponya wagonjwa, kuyafungua macho ya vipofu, kwa ule uweza mkuu mno anajithibitisha kuwa yeye yule daima. Haleluya!

¹⁵⁰ Msifuni. Inueni mikono yenu. Sahau mahali mlipo; jueni tu kwamba mko karibu na Yeye, na wema Wake, na utukufu Wake, na nguvu Zake, na rehema Zake zinadumu milele. Ni Yeye yule daima. Jina la Bwana libarikiwe. Haleluya! Loo, lisifuni Jina Lake Takatifu.

¹⁵¹ Loo, Yeye ni wa ajabu jinsi gani, yuna nguvu jinsi gani. Ni wangapi wangetaka kuyaweka maisha yenu wakfu kwa Mungu sasa hivi, upya? Inua mkono wako. Ni wangapi wangetaka kuyaweka maisha yenu wakfu kwa Mungu? Jambo ndilo hilo. Inueni mikono yenu. Hebu tuone Pentekoste. Hebu tuwaone watu wa Mungu. Nitainua mkono wangu. “Bwana, mimi hapa. Nitume mimi.” Mchukue Malaika basi mwenye makaa ya madhabahuni na uzitume nguvu Zako juu yetu, Bwana. Mungu, tujalie katika utimilifu wa Roho Wako, Ee Baba. Yasikie maombi yetu, Ee Bwana. Yasikie maombi yetu, kama watoto waaminio wanaosimama. Jina Lake lisifiwe.

¹⁵² Loo, kama mawimbi ya utukufu yanayoshuka, loo, matone ya umande wa rehema. Ee, Mungu asifiwe. Nafsi zetu na zingojee. Je! mnasadiki hayo? Je! mnasadiki hayo? Huyu ni Roho Mtakatifu ajaye. Hizi ndizo nguvu zisizoonekana zinazotuingiza katika Ufalme wa Mungu, zile baraka za Pentekoste. Rudini nyumbani. Mnatarajiwa kurudi nyumbani. Ninyi ni watu wa thamani. Mungu anawataka mjiweke wakfu. Enyi wanawake, jisafisheni. Wanaume, jisafisheni. Hebu tuanze kumrudia Mungu na kumtumikia Mungu kwa moyo safi kabisa.

¹⁵³ Msifuni Mungu, Roho Mtakatifu amejitokeza mkutanoni. Fanyeni tu yale mnayojisikia kuongozwa kufanya. Acheni tu Roho Mtakatifu atende kazi juu yenu. Hakuna jambo ninaloweza kusema. Sijui niseme nini sasa. Roho Mtakatifu yumo kote jengoni. Jina la Bwana libarikiwe. Bwana asifiwe. Loo, Haleluya! Haleluya! Sifa kwa Bwana. Bwana asifiwe. Ni ajabu jinsi gani, ni tukufu jinsi gani. . . Zinapendeza, ni nzuri jinsi gani sifa za watakatifu wa Bwana juu ya nyuso zenu, kwenye Uwepo wa Roho Mtakatifu hapa ukitenda kazi na kutuonyesha utukufu Wake kutoka kwenye umati huu wenye moyo mmoja, ukilisifu Jina Lake.

¹⁵⁴ Geuka moja kwa moja na kupeana mikono na mtu fulani, useme, “Bwana asifiwe, ndugu. Bwana asifiwe, dada.” Hebu tuingie ndani kabisa na kumruhusu Mungu atuchochee. Bwana asifiwe. Hiyo ni sawa. Ninyi Wamethodisti wote, na Wabaptisti, na Wapresbiteri, Wapentekoste, na Wasabato, na wowote wale, peaneni mikono Mbele za Bwana Mungu. Jambo ndilo hilo. Loo,

Haleluya! Haleluya! Haleluya! Loo, nina furaha sana mimi ni mmoja wao. Nina furaha sana. Loo, kubomoa kuta, kutupilia mbali takataka. Utukufu! Uhuru katika Bwana, kulisifu Jina Lake takatifu. . . Jina la Bwana lisifiwe. Loo, Haleluya! Bwana asifiwe.

¹⁵⁵ Loo, napenda tu kuona hilo: watu wakipeana mikono na kuzinawirisha nyuso zao. Nguvu za Mungu zikisema, “Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo, sisi ni watoto wa Mungu. Sisi sote ni kanisa moja kubwa mno, mtu mmoja mkubwa mno katika Kristo Yesu, Bibi-arusi Wake, Mwenye utukufu.” Kuja kwa Bwana kunakaribia. Watu Wake wanakusanyika pamoja na kupendana. . . kwa upendo na nguvu za Uwepo Wake. Loo, hii ni kama Mbinguni. Loo, hii ni nzuri. Amina. Loo, ni tukufu jinsi gani, ni ajabu jinsi gani: kumwabudu tu Bwana katika Roho na katika nguvu. Ni wakati wa jinsi gani. (Hicho kilikuwa kikome; tunaanza.)

¹⁵⁶ Hakuna tu ninii. . . Niliwaambia ndugu, “Ndugu, hakuna mahali pa kusimamia.” Hakuna mahali hapa ambapo. . . Kamwe hatukuanza, kwa hiyo hatukomi. A—ajabu tu. . . Ni wangapi wanajisikia vizuri sana? Uwepo tu wa Bwana, loo, jamani, ni wa ajabu, Uwepo wa Bwana hapa.

¹⁵⁷ Sasa, Uwepo wa Bwana upo hapa kuwaponya wagonjwa, kuwapa watu afya. Mwaminini tu. Mnamwamini? Kama tunaweza kumwamini, mambo yote yanawezekana. Mnaamini hilo? Mnaamini ya kwamba huo ni Uwepo wa Bwana?

¹⁵⁸ Sasa, wakati mkininii. . . Nipeni tu muda kidogo, muda kidogo tu sasa, na msikilize kwa muda kidogo tu. Hebu niwathibitishie ni Roho Mtakatifu hapa. Hebu niwaonyeshe ya kwamba Roho Mtakatifu, Yeye yule anayenena, Yeye anayefanya jambo hili, anajua hilo. Ni wangapi waliopo hapa sasa, waliokuja hapa wagonjwa? Hebu tuone mikono yenu. Wale waliokuwa na ugonjwa. . . Kuna watu. . .

¹⁵⁹ Yupo mtu anayesimama hapo. Unaamini, bwana? Hakuna kadi za maombi zilizosambazwa, bali je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Unaamini anaweza kuniambia shida yako? Ipo ubavuni mwako. Umpangiwa upasuaji. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bw. Cartwright. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Punga mkono wako. Vema. Nenda nyumbani na uwe mzima, hutauhitaji. Unaamini hilo?

¹⁶⁰ Huyu mwanaume anayemshika huyo mtoto mchanga mikononi mwake, je! unaamini kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu? Unaamini huyu kwamba ni Roho Mtakatifu? Sikujui, hiyo ni kweli? Sijapata kukuona maishani mwangu; hatufahamiani. Unaamini Roho Mtakatifu anaweza kuniambia mtoto huyo mchanga ana shida gani? Ana ukurutu. Hiyo ni kweli. Sivyo? Hakika. Hutoki hapa. La. Una ugonjwa wa tumbo, unaokusumbua, wewe mwenyewe. Hiyo ni kweli, sivyo?

Umetoka kwenye Jiji la Kansas. Vema. Rudi, Yesu Kristo anakuponya. Haleluya! Wewe amini. Unaamini kwa moyo wako wote?

¹⁶¹ Huyu hapa Malaika wa Bwana, akizungukazunguka juu ya ma—maskini mwanamke huyu, mzee mwema, anayeketi hapa ndani, akiugua ugonjwa wa ngiri. Unaamini Mungu atakuponya hiyo ngiri, dada? Wewe, mwenye ua dogo jekundu kwenye kofia yako, inua mkono wako. Vema. Nenda nyumbani na upate afya. Amina. Loo, ni Mungu; ni Kristo Mwana wa Mungu. Amefufuka katika wafu. Yupo hapa.

¹⁶² Sasa, wekeaneni mikono na mwombe dua nzuri ya msimu, kila mmoja wenu, wakati nikimwomba mtu fulani aje hapa. Njoo hapa, ndugu. Wakati mkiwekeana mikono kuonyesha kwamba Mungu huponya pia, nitamwomba ndugu hapa aombe dua pia. (Endelea. Vema.) Bwana Mungu asifiwe. 

JE! UNASADIKI HAYO? SWA60-0402

(Believest Thou This?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi, tarehe 2 Aprili, 1960, katika Jumba la Mikutano la Manispaa huko Tulsa, Oklahoma, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org